

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

Simu: +255262963309/13/14
Nukushi: +255 262 963 316
Barua pepe: ps@lands.go.tz
Tovuti: www.lands.go.tz



Mji wa Serikali, Mtumba,
S. L. P. 2908,
40477 DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

KUHUSU ULIPAJI WA KODI YA PANGO LA ARDHI

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inapenda kuwajulisha wananchi wote kuwa, kwa mujibu wa **Fungu la 33 (1) la Sheria ya Ardhi (Sura ya 113)**, kila mmiliki wa ardhi amepewa sharti la kulipa Kodi ya Pango la Ardhi kwa kila mwaka.

Aidha, kwa mujibu wa **Fungu la 44 (1) la Sheria ya Ardhi (Sura ya 113)**, kila mmiliki wa ardhi anatakiwa kutimiza masharti ya umiliki ikiwa ni pamoja na sharti la kulipa Kodi ya Pango la Ardhi. Kitendo cha kutolipa Kodi ya Pango la Ardhi ndani ya muda uliowekwa na sheria, kinasababisha mmiliki wa ardhi kuvunja moja ya sharti la umiliki.

Wizara kwa nyakati tofauti, imekuwa ikihamasisha na kuwakumbusha wamiliki wa ardhi kulipa Kodi ya Pango la Ardhi. Hata hivyo, baadhi ya wamiliki wa ardhi hawajatekeleza wajibu huo wa kisheria. Hivyo, naelekeza wamiliki wote wa ardhi wanaodaiwa Kodi ya Pango la Ardhi, kulipa kodi husika ndani ya siku thelathini (30) kuanzia tarehe ya tangazo hili. Baada ya muda huo kupita, hatua za kisheria zitachukuliwa katika maeneo yafuatayo:-

- a) Kwa mujibu wa **Fungu la 50 la Sheria ya Ardhi (Sura ya 113)**, wamiliki hao watafikishwa mbele ya Mahakama; na
- b) Kwa mujibu wa **Fungu la 45 la Sheria ya Ardhi**, taratibu za kisheria za ubatilisho wa milki zao zitaendelea.

Katika kipindi hicho cha siku thelathini (30), vituo vya makusanyo ambavyo ni; Ofisi za Ardhi za Mikoa na Ofisi za Ardhi za Halmashauri zote nchini, kwa siku za kazi zitakuwa wazi hadi muda wa saa 2:00 Usiku. Hivyo, naagiza watendaji wote wa Sekta ya Ardhi, kuratibu mazingira rafiki kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa mkakati huu.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Jerry William Silaa'.

Jerry William Silaa (Mb.)

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

10 Mei, 2024